
Bunge la Taifa la **Wales**

# Mwongozo Wako wa Bunge







Swahili




**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Laini ya maelezo: 029 2089 8200

Laini ya kufanya miadi: 029 2089 8477

Simu ya maandishi: 029 2089 8261


Kijitabu hiki cha maelezo kinapatikana pia ukiomba katika fomati zifwatazo:

Chapa kubwa • Breli • CD • Lugha ya Ishara ya Uingereza (BSL)

Kinapatikana pia kielektroniki kwa www.wales.gov.uk katika lugha zifwatazo:

Kiarabu • Kibengali • Kifarsi • Kifaransa • Kigujarati • KIhindi • Kiholanzi • Kiitaliano • Kiingereza • KiJapani • Kikantonisi •Kireno • Kisomali • Kiswahili • Kiujerumani • Kiuspania • Kiurdu • Kiwelshi

Utafsiri wa simu unapatikana katika lugha 60 kwa watu ambao lugha yao ya kwanza si Kiingereza au Kiwelshi. Ili kufikia huduma hii, piga simu 029 2089 8200 na uashirie lugha ya chaguo lako. Opareta atakuunganisha na mtafsiri.


Barua pepe (kawaida): assembly.info@wales.gsi.gov.uk

Barua pepe (kufanya miadi): assembly.booking@wales.gsi.gov.uk

Public Information and Education Service
National Assembly for Wales
Cardiff CF99 1NA


Kwa maelezo mapya kabisa tembelea tovuti ya Bunge kwa
**www.wales.gov.uk**

Tazama bunge moja kwa moja kwenye kompyuta yako ya kibinafsi kwa
**www.webcasting.wales.gov.uk**


APS/017/8/03.06

ISBN Nambari ya: 0 7504 9724 6



Crown copyright 2006

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| **Usuli wa Bunge** | 4 |
| **Bunge** | 4 |
| **Maisha ya usoni ya Bunge** | 4 |
| **The Senedd [Seneti]** | 5 |
| **Vile Bunge inavyoteuliwa** | 6 |
| **Mikoa na maeneo ya uchaguzi** | 7 |
| **Nani ni nani katika Bunge** | 8 |
| Afisa Mkuu | 8 |
| Waziri wa Kwanza wa Wales na Bunge la Serikali ya Welsh | 8 |
| **Mjadala** | 9 |
| **The Siambr [Chumba cha Baraza la Wabunge]** | 10 |
| **Kazi ya Kamati za Bunge** | 10 |
| Kamati za Hoja | 10 |
| Kamati za Sheria | 11 |
| Kamati za Shughuli | 11 |
| Kamati za Bunge | 11 |
| Kamati za Mkoa | 11 |
| Kamati za Ziada | 11 |
| Kufanya kazi pamoja na Kamati ya Mambo ya Wabunge wa Welsh | 11 |
| **Kufikia Bunge** | 12 |
| Mjadala na Kamati | 12 |
| Kutangaza Matukio ya Bunge | 12 |
| Vituo vya Wageni na Maonyesho | 12 |
| Bunge katika Mikoa | 12 |






## Usuli wa Bunge

Mnamo Julai 1997, Serikali ya Uingereza ilichapisha Karatisi nyeupe, ripoti ya serikali inayopeana mapendekezo *A Voice for Wales [Sauti ya Wales]*, ambayo ilifafanua mapendekezo ya ugawanyishaji  katika Wales. Mapendekezo haya yalipitishwa katika kura ya maoni mnamo Septemba 18 1997. Bunge pia ilipitisha Government of Wales Act 1998 [Sheria ya Serikali ya Wales ya 1998], ambayo iliimarisha Bunge la Taifa la Wales.

The National Assembly for Wales (Transfer of Functions) Order 1999 [Amri ya 1999 ya Bunge la Taifa la Wales [Ubadilishanaji wa Wajibu] iliwezesha ubadilishanaji wa uwezo uliogawanywa na wajibu kutoka kwa Katibu wa Jimbo la Wales hadi kwa Bunge mnamo tarehe 1, julai 1999. Vivyo hivyo, Sheria nyingi za Bunge zimepeana uwezo mpya kwa Bunge.

## Bunge

Bunge uamua vipaumbele vyake na kutenga fedha zinazopatikana kwake kutoka kwa Hazina ya Serikali ya uingereza (au Wizara ya Fedha). Kati ya uwezo wake uliogawanywa, Bunge ukuza sera na ukubali utungaji sheria ambao unaonyesha mahitaji ya watu wa Wales. Uamuzi kuhusu maswala haya yanafanywa na wale waliochaguliwa ofisini na watu wa Wales. Wales hubakia sehemu ya Uingereza, na Katibu wa Jimbo la Wales na Wanabunge (MPs) kutoka mikoa ya Welsh huendelea kuwa na viti katika Westminister. Sheria ambazo zinapitishwa na Bunge katika Westminster bado hutumika kwa Wales.

Utungaji wa sheria za kando, ambazo hupeana maelezo ya vile hali ya Sheria ya Bunge itatumika, ndio kazi kuu ya Bunge. Sheria kuu iliyofanywa na Westminster Parliament [Bunge la Westmister] Hupangilia uwezo wa Bunge wa kutunga sheria za kando. Hii inamaanisha kuwa Sheria ya Bunge inaweza kuwa na madhara tofauti katika Wales kwa ile ya uingereza. Kwa mfano, mnamo Octoba 1 2004 Bunge iliweka kiwango chake chenyewe cha malipo ya maagizo ya madawa katika Wales, tofauti na malipo inayotumika katika Uingereza.

## Maisha ya usoni ya Bunge

Kwa sasa Bunge la Taifa lina uwezo ulio na mipaka peke yake na mpangilio wake sio wa kawaida na serikali yake (kuu) na bunge (utungaji sheria) ikiungana kama shirika moja[1] chini ya kichwa cha ujumla cha  'The National Assembly for Wales' [Bunge la Taifa la Wales]. Katika mashirika mengi ya bunge, ikihusisha Westminster and Bunge la Scottish, serikali na watunga sheria wako kando kisheria.

Mnamo Julai 17 2005, Katibu wa Jimbo la Wales, Mheshimiwa Peter Hain MP, alileta karatasi nyeupe iliyoitwa 'Better Governance for Wales' [Utawala Mzuri wa Wales]. Karatasi hii Nyeupe iliweka mapendekezo ya Serikali kwa ajili ya utungaji wa sheria ili kubadilisha hali ziliopo sasa katika Sheria ya Serikali ya Wales kwa vipengele vitatu:

- Kubuni mpangilio mpya wa serikali ya Bunge;
- Kuongeza uwezo wa kutunga sheria za Bunge;
- Kubadilisha mfumo wa uchaguzi.

Hii itamaanisha kuwa bunge na bunge ya serikali itakuwa kando kirasmi. Mswada wa kufanya mabadiliko unaendelea sasa kupitia Bunge na unatarajiwa





kuwa sheria kabla ya mwisho wa 2006. Tukikisia mswada huu utapitishwa katika hali yake iliyopendekezwa, Mabadiliko kwa Bunge yatatekelezwa baada ya uchaguzi unaofwata kufanyika mnamo tarehe 3 Mei 2007.

Kwa sasa Bunge imeanza kufanya kazi kuwadia kufanya mabadiliko kati ya utungaji sheria uliopo na, haswa, kugawanya serikali yake na watunga sheria kama iwezekanavyo. Hii itafanya kuwa rahisi kwa watu kuelewa kazi ya Bunge na Serikali, na pia kusaidia kuongeza uwajibikaji wa kidemokrasia.

Maelezo juu ya Karatasi Nyeupe na Mswada inaweza kupatikana kwa tovuti ya Wales Office [Afisi ya Wales] kwa **www.walesoffice.gov.uk**

(1) Shirika moja = Bunge la Taifa la Wales (wanachama 60 waliochaguliwa katika uchaguzi wa Bunge la Taifa la Wales kila miaka nne) na Bunge la Serikali ya Welsh (wanachama wa Bunge waliochaguliwa wa chama ilio na watu wengi) inajumuisha shirika moja linalojulikana kama 'Bunge la Taifa la Wales'.

## The Senedd [Seneti]

Jengo jipya la Bunge la Taifa la Wales, the Senedd [Seneti], liko mahali panapoonekana palipo zungukwa na maji katika Cardiff Bay. Ni jengo la kitofauti, ambalo liliundwa na Richard Rogers Partnership ili kuonyesha filisofia kuu ya Bunge la Kitaifa ya wazi na uadilifu.

Jengo hili limeundwa ili kufikia viwango vikuu vya kazi ya mazingira. Utumiaji wa nguvu na upotezaji unapunguzwa na utumizi wa teknolojia ya kubadilisha upya. Muundo huo unahusisha vifaa vya asili.



# Vile Bunge inavyoteuliwa

Kuna Wanachama wa Bunge 60 (AMs). Uchaguzi ufanywa kila miaka nne na wapiga kura wana kura mbili.


Kati ya hao wanachama 60, 40 wanawakilisha mikoa na wanachaguliwa kulingana na mfumo wa yule aliye na kura nyingi, mfumo ambao wanachama wa Bunge wanachaguliwa Bungeni.

Wanachama wengine 20 wanawakilisha maeneo ambayo yako sawa na mikoa ya Bunge ya Uropa. Wanachama wa maeneo wanachaguliwa kwa njia ya uwakilishishaji sawa unaojulikana kama Additional Member System [Mfumo wa Kuongeza Mwanachama]. Mfumo huu uhakikisha kuwa kwa jumla nambari ya viti  ambavyo vinashikiliwa na kila chama cha kisiasi vinaasharia kiwango cha kura ambazo chama hicho kimepokea.

Kila eneo la uchaguzi linafunika kati ya mikoa 7 hadi 9.Kuna Wanachama wa Bunge 4 wa eneo wanaochaguliwa kwa kila maeneo 5.

Maeneo haya 5 ya uchaguzi ni:

- Wales ya Kaskazini;
- Wales ya Kati na Magharibi;
- Wales ya Kusini Mashariki;
- Wales ya Kusini Magharibi;
- Wales ya Kusini ya Kati.




Mpaka wa Mkoa wa Bunge

Mpaka wa Eneo la Uchaguzi wa Bunge

# Mikoa na maeneo ya uchaguzi





# Nani ni nani katika Bunge

## Afisa Mkuu

Afisa Mkuu anachaguliwa na wanachama wote wa Bunge. Baada ya kuchaguliwa, Afisa Mkuu hatumikii Bunge kabisa. The Deputy Presiding Officer [Afisa Mkuu Msaidizi] anachaguliwa kwa njia hiyo pia.

Kazi kubwa ya Afisa Mkuu ni kuongoza Mjadala, kuweka mpangilio na kulinda haki za wanachama wa Bunge. Ni jukumu ya Afisa Mkuu kuhakikisha kuwa shughuli zimeshughulikiwa kwa msingi wa usawa na bila upendeleo. Afisa Mkuu anawajibu wa Standing Orders(2) [Sheria za Bunge] na yeye ndiye ana mamlaka ya mwisho kuhusu utafsiriwa wa sheria hizo.

Afisa Mkuu pia uongoza mikutano ya Jopo la wenye kiti, ambapo mpangilio wa kamati na maswala yanayodhuru shughuli za kamati hujadiliwa na kila mwenye kiti wa kila Kamati.

Afisa Mkuu Msaidizi husaidia kama iwezekanavyo Afisa Mkuu na yeye ndiye Mwenye kiti wa Bunge.

## Waziri wa Kwanza wa Wales na Bunge ya Serikali ya Welsh

Wanachama 60 wa Bunge hupeana uwezo wao mkubwa, ikihusisha utekelezaji wa sera na utungaji wa sheria kwa Waziri wa Kwanza wa Wales, ambaye huchaguliwa na Bunge lote na kwa hivyo huwa kiongozi wa chama kikubwa kabisa cha kisiasa au vyama. Waziri wa Kwanza naye hupeana jukumu la kupeana kazi za serikali kwa Mawaziri wa Bunge la Serikali ya Welsh, ambao kwa pamoja uunda Baraza la Mawaziri.

Baraza la Mawaziri hufanya uamuzi mwingi wa bunge wa siku baada ya siku, na Mawaziri wake wanawajibu wa maeneo ya maswala yafuatayo:

- Elimu, Mafunzo ya Muda mrefu na Utaalamu;
- Biashara, Ubunifu na Mitandao;
- Mazingira, Upangaji na Mashambani;
- Afya na Huduma za Jamii;
- Fedha, Serikali ya Mitaa na Huduma za Umma;
- Tamaduni, lugha ya Welsh na Michezo; na
- Haki za Kijamii na Wongofu.

The Cabinet [Baraza la Mawaziri] wana uwajibikaji kwa Bunge, ambayo huchunguza uamuzi wake na hatua zake.

(2) Sheria za Bunge = amri ambazo Bunge la Taifa la Wales hutumia.

# Mjadala

Plenary is a meeting of all Assembly Members which takes place in the Siambr. Mjadala ni mkutano wa wanachama wote wa Bunge ambao hufanyika katika Siambr [chumba cha Baraza la Wabunge]. Ni mazungumzo ya Bunge ya kufanya uamuzi na kutunga sheria. Mjadala huu hufanyika Jumanne na Jumatano jioni adharani na utangazwa moja kwa moja kwa kituo cha runinga cha S4C 2.

Afisa Mkuu uchapisha ajenda ya kila mkutano mapema. Shughuli ushughulikiwa kwa mpango ambao unaonekana kwa ajenda. Kwa kila wiki Bunge upatana ili kujadili, dakika 45 hupeanwa kwa Maswali ya Kusema kwa Waziri wa Kwanza. Kwa kuongezea, kila Waziri wa Baraza hujibu Maswala ya kusemwa mara moja kwa kila wiki nne. Wanachama wa Bunge hujadili maswala yalio kwa ajenda na kupigia kura mapendekezo yaliyopenwa.

Kwa idhini ya Afisa Mkuu, Mwanachama wa Bunge anaweza kusema kuwa mara moja Bunge izingatie swala la umma la maana la haraka. Mwanachama wa Bunge anaweza pia kusema swala lijadiliwe kwa ufupi kabla ya mjadala kuisha.



Muda hupeanwa katika kipindi cha Mjadala kwa vitengo fulani vya shughuli za Bunge, kama vile:

- Kuwekwa kando bajeti ya Bunge;
- mapendekezo yaliyopeanwa kwa niaba ya vikundi vya kisiasa ambavyo havijawakilishwa katika Baraza la Bunge;
- ripoti zilizopeanwa na Kamati ya Maswala na Mkoa; na
- maswala yanayo husiana na Umoja wa Uropa.







## The Siambr [Chumba cha Baraza la Wabunge]

Kila mwanachama wa Bunge ana kiti kilichotengwa katika Chumba cha Baraza la Wabunge ambacho kina kompyuta iliyo na skrini ya kugusa ambayo wanaweza kufikia wakati wa mijadala. Mfumo wa 'Chamberweb' unawawezesha wanachama wa Bunge kufukia barua pepe na maelezo.

Bunge lina lugha mbili na Wanachama wa Bunge wanazungumza lugha yao wanaoipendelea, Kiingereza au Kiwelshi. Utafsiri, Welshi kwa Kiingereza, inapeanwa kwa mijadala yote na mikutano yote ya Kamati.

Washirika hupiga kura kwa kubofya kiweko kwenye madaftari yao. Wanaweza kuchagua kupiga kura "Yes," [ndio] "No" [hapana] au "Abstain" [Kutopiga kura]. Matokeo huonyeshwa papo hapo kwenye skrini ndani ya Chumba hicho.

Rekodi ya maneno ya matukio utolewa kwa kila Mjadala, Kamati ya Hoja na Kamati ya Sheria, uhariri ili iwe sahihi, kamili na kuepuka kurudia kusikohitajikana. Hii ni chanzo cha maelezo ambacho kinaweza kufikiwa na wote. Nakala za lugha mbili ya matukio huchapishwa kwenye tovuti ya Bunge kati ya masaa 24 ya kila Mjadala. Maelezo haya yanapatikana pia ukiomba katika chapa kubwa, Breli na kwa (CD).

Ili kutazama Rekodi za Matukio, tembelea tovuti ya Bunge kwa **www.wales.gov.uk/keypubrecordproceedings/index.htm**

## Kazi ya Kamati za Bunge

Kamati ya Bunge ni kikundi cha wanachama wa Bunge ambao hupatana kila wakati ili kuchunguza sera na utungaji wa sheria. Kamati kwa kawaida huwa 'zinalingana kichama' zikionyesha nambari ya Wanachama wa Bunge wanaowakilisha kila chama katika Bunge. Kamati nyingi hupatana adharani. Kamati ambazo hupatakana faraghani ni Kamati ya Shughuli na Kamati ya Bunge. Kamati ya Bunge hupatana adharani mara moja kwa mwaka. Kamati juu ya Viwango za tabia inaweza kuamua kujadili malalamishi kwa faragha. Kamati zingine wakati mwingine hupatana kwa faragha ili kuzingatia mambo fulani ya ajenda.

### Kamati za Hoja

Kamati za hoja husaidia kukuza sera, kushauri kuhusu utungaji wa sheria za kwanza, za pili na za Uropa na kuchunguza kazi ya Mawaziri. Wanachama wa Bunge kutoka kwa vyama vyote wanaweza kujadili maswala na kushiriki maoni kuhusu vile Bunge inavyofanya kazi. Kila Kamati ya Hoja huangalia uwaziri wa Waziri wa Baraza, ambaye ni mwanachama wa Kamati.

Kamati za Bunge za Hoja ni:

- Elimu, Mafunzo ya Muda mrefu na Utaalamu;
- Biashara, Ubunifu na Mitandao;
- Mazingira, Upangaji na Mashambani;
- Afya na Huduma za Jamii;
- Fedha, Serikali ya Mitaa na Huduma za Umma;
- Tamaduni, lugha ya Welsh na Michezo; na
- Haki za Kijamii na Wongofu.

## Kamati za Sheria

Kamati tano za Sheria ni:

- Kamati ya Ukaguzi wa Mahesabu – ambayo ukagua utumiaji wa rasilimali ya Bunge;
- Kamati ya Nafasi Sawa – ambayo uchunguza shughuli za Bunge ili kukuza nafasi sawa;
- Kamati ya Uropa ya Mambo ya Nje – ambayo uzingatia mambo ya Umoja wa Uropa inayodhuru Wales na kazi pana ya 'Wales ulimwenguni';
- Kamati ya kutunga Sheria – ambayo ukagua utungaji wa sheria zinazoletwa mbele ya Bunge; na
- Kamati ya Viwango za Tabia -ambayo usimamia viwango vya tabia za Wanachama wa Bunge na kuchunguza malalamishi kuhusu ukeukaji wa tabia au ukeukaji wa amri.

## Kamati ya Shughuli

Kamati ya Shughuli, inayojumuisha mmoja wa Mwanachama wa Bunge kutoka kwa kila chama cha kisiasa, humshauri Waziri wa Shughuli kuhusu usimamizi wa shughuli za bunge; humshauri Afisa Mkuu Msaidizi kuhusu njia ya kutunga sheria za kando; na huzingatia kazi ya kawaida na mpangilio wa Bunge katika utekelezaji wa shughuli zake.

## Kamati ya Bunge

Bunge imepeana uwezo wa juu kwa Kamati ya Bunge. Kamati hii inaongozwa na Afisa Mkuu Msaidizi na hushughulika na mambo yanayohusiana na huduma ya Wanachama wa Bunge. Hii inajumuisha:

- huduma, vifaa and malazi;
- Marupurupu ya Mwanachama ya kifedha; na
- Mambo yanayohusiana yanayosaidia kazi ya Bunge.

## Kamati za Mkoa

Kuna kamati tano za Mkoa. Wanachama wa Bunge wa Mkoa na Maeneo uunda kila Kamati ya Mkoa. Wanachama wa Kamati husikiliza maoni ya jamii za mtaa ili kuhakikisha kuwa Bunge inawakilisha Wales yote.


## Kamati za Ziada

Bunge linaweza kuamua kuanzisha kamati zisizodumu za ziada ili kuzingatia maswala nyeti kati ya makubaliano yaliyokubaliwa na Bunge. Mifano inajumuisha Kamati ya Uvutaji Sigara katika Sehemu za Umma na Kamati ya Kugharamia Shule.

## Kufanya kazi pamoja na Kamati ya Mambo ya Wabunge wa Welsh

Sheria za Bunge katika Bunge la London na Bunge la Taifa la Wales la Cardiff uruhusu kufanya kazi pamoja kati ya Kamati ya Mambo ya Wabunge ya Welsh na Kamati zingine za Bunge.





# Kufikia Bunge

## Mjadala na Kamati

Watu wa umma wamekaribishwa kuudhuria Mjadala na mikutano ya Kamati ya umma. Mjadala na Kamati nyingi za Sheria na Hoja hufanyika kwa jengo la Bunge katika Cardiff Bay na maelezo uchapishwa kwa tovuti ya Bunge. Kamati za Mkoa hufanyika mara kwa mara katika jamii za mtaa kila mahali katika Wales na maelezo uchapishwa katika gazeti la kawaida na katika vyombo vya habari.

## Kutangaza Matukio ya Bunge

Mijadala yote na mikutano mingine ya Kamati hutangazwa moja mwa moja kwenye kituo cha S4C2 cha runinga ya dijiti. Mikutano ya moja kwa moja na iliyohifadhiwa inaweza kutazamwa kupitia tovuti kupitia **www.webcasting.wales.gov.uk**

## Vituo vya Wageni na Maonyesho

Bunge lina vituo viwili vya Wageni na Maonyesho. 'The Assembly at the Pierhead' [Bunge katika PierHead] liko katika jengo la Pierhead katika Cardiff Bay na Kituo cha Wageni cha Wales Kaskazini kiko katika Colwyn Bay.

Vituo hivi huwapa wageni fursa ya kujifunza, ambao imeundwa ili kufanya kusoma kuhusu Bunge kuwa ya kupendeza na ya kuhusisha. Maonyesho yanapeana maelezo kuhusu Bunge na kazi yake na wajibu wake katika Wales, na huwapa wageni fursa ya kufikia maelezo mapya kabisa juu ya nani ni nani, kile kinachotendeka na vile Bunge hufanya kazi. Vituo vyote vina maduka yanayopeana vifaa vya aina kadhaa vilivyopigwa chapa kutoka Wales yote. Wageni wanakaribishwa waweze kutembelea Vituo hivi au kupanga miadi ya safari mapema.

## Bunge katika Mikoa

Bunge imejitolea kuwafikia watu wote wa Wales. Wafanyakazi wa Huduma ya Bunge wako katika mikoa ili kukuza uhusiano na jamii ya mtaa na vikundi vya mkoa kwa kuhudhuria hafla zao na maonyesho. Kwa kuwa hapo kwenye hafla na viwanjani, wafanyakazi wanaweza kuendeleza kazi ya Bunge na kupatana na watu wa mtaani na kutafuta maoni yao.